
# NGURUMO ya MWANDISHI

Toleo LA VI-Machi-MMXXII



Kusoma ni kuzaliwa upya...

Kusoma ni kuzaliwa upya...

# KUSOMA NI KUZALIWA UPYA

ASALAAM ALEIKUM ndugu wapenzi wa Ngurumo ya Mwandishi. Ni mara nyingine tena tunakujia katika toleo hili la sita la jarida letu.

Kwanza nipende kukushukuruni sana kwa kulipokea, kulisoma na kulisambaza kwa marafiki zetu. Nimepata meseji za Whatsapp kutoka Burundi, Kenya, Marekani na Uganda. Hii inaonesha wazi kuwa wasomaji wetu mnafanya kazi kubwa ya kututangaza.

Tumepokea pia maoni yenu na wadau mbalimbali wa jarida hili ya nini kiboreshwe na kipi kiwekwe vipi katika matoleo yajayo. Napenda tu kuwaambia kuwa maoni yenu yametufikia na yanafanyiwa kazi. Hivyo kidogo kidogo tutaanza kuyafanyia kazi.

Katika toleo hili la mwezi wa Machi, Dawati la Mhariri la Ngurumo ya Mwandishi linakwambia kuwa KUSOMA NI KUZALIWA UPYA. Kivipi? Sote tunajua kuwa kiumbe chochote kinapozaliwa basi ni wakati wa kujua na kujifunza mambo mapya. Vivyo hivyo kwa kusoma vitabu na majarida anuai ni sawa na kuzaliwa upya kwani ni wakati wa kujifunza mambo mapya.

Kama vile sisi tunavykusisitiza kusoma basi nawe wasisitize wengine wasome ili waone faida yake.

Ni jambo zuri kila upatapo nafasi kutembelea maktaba ama ya shuleni kwako au wilaya hata ya mkoa ili uweze kujifunza na kuongeza maarifa zaidi katika maisha yako.

Je wewe wafanya hivyo? Kama ndiyo, basi kongole nyingi kwako na ongeza zaidi bidii ukiwachukua na rafiki zako.
Na kama hii si tabia yako basi anza kidogokidogo kwenda kutembelea maktaba na mwisho utaona mabadiliko kwenye maisha yako. R.M

## MWANDISHI WETU: HASSAN MBONECHE




JINA langu ni Hassan Mboneche, mzaliwa wa Mangaka mkoani Mtwara. Lakini kwa sasa makazi yangu ni Moshi, mkoani Kilimanjaro.

Kwa muda mrefu nimekuwa mpenzi, shabiki na mdau wa kazi za Sanaa, hasa uandishi. Mapenzi yangu kwa sanaa ya uandishi ndiyo yaliyochangia kunipa hamasa ya nami kuwa mwandishi wa kazi bunilizi hususan uandishi wa riwaya.

Kama ilivyo kawaida ya wengi, huanza wakiwa na ufahamu mdogo, ndivyo ilivyokuwa kwangu pia. Lakini leo hii nimepiga hatua, inayofanya maandishi yangu yang'ae. Kwa hilo sina budi kuwashukuru waandishi wenzangu na wasomaji pia. Na kwa dhati kabisa, natoa shukrani kwa wanachama wenzangu wa UWARIDI.

Umoja huu umenijenga kwa mengi, mojawapo ni kunipa mwongozo bora wa uendeshaji wa kazi zangu.

Kuhusu kazi nilizofanya, mpaka sasa nina kitabu kimoja sokoni kiitwacho Nenda. Ambacho ni riwaya ya mapenzi inayomzungumzia msichana mjamzito aliyetelekezwa na mpenziwe katika mazingira tata huku akiachiwa mzigo unaomlazimu kuukabili.

Mbali na hiyo, nina kazi zingine ambazo nataraji kutoa moja baada ya nyingine kadiri muda utakavyoruhusu. Na kazi tarajiwa ni Waraka. Riwaya ya kipelelezi inayohusisha uhasimu wa vikundi viwili vya kijeshi; SWATTA kutoka jeshi la polisi, na SCOT kutoka jeshi la ulinzi. Kazi zote hizi hupatikana nchi nzima, kupitia kwa mawakala. Kwa wanaohitaji kufuatilia kazi hizi, wanaweza ku-Like ukurasa wangu wa kijamii uitwao Tanuru la Simulizi kwa taarifa mbalimbali.

Mwisho, natoa wito kwa waandishi wenzangu, tuamini katika ushirikiaano kwa ufanisi mzuri wa tasnia yetu. ***H.M***

# MAKTABA YA MKOA IRINGA NA MPANGO WA KUINUA WAANDISHI

**Na Mwandishi wetu**

**Mpango wa kuinua na kusaidia uandishi na waandishi mkoani Iringa umekuwa wazo kuu la maktaba ya Mkoa huo.**

Kongamano lililowakutanisha waandishi wa maudhui anuai lililoandaliwa na maktaba hiyo limekuwa chachu ya kuanzisha chama kinachowaunganisha waandishi hao.

Akizungumza na mwandishi wa jarida hili, Mkutubi Kiongozi wa maktaba mkoani humo Bi. Consolatha Muingereza alieleza kuwa mkoa wa Iringa una utajiri wa waandishi lakini bado changamoto ni kuwa hawajui wafuate hatua gani. Hakuishia hapo, aliendelea kusema kuwa wasomaji wa mkoa huo wangependa kuona machapisho ya waandishi wao yakiwa maktaba hapo.

Kongamano hilo lililochagizwa na wanazuoni kutoka vyuo vikuu vya RUCU na IRINGA (Tumaini) liliibua wazo moja kubwa la kuanzisha chama cha waandishi chenye lengo la kuwaunganisha na kuwainua mintarafu kuwasaidia katika maswala ya uandishi.

Mgeni rasmi katika kongamano hilo, Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Mh. Queen Cathbert Sendiga alisema kuwa "Kuandika habari au vitabu hakukufanyi uache kusoma. Uandishi unatakiwa tafiti".

Mkuu wa mkoa huyo aliyekubali kwa roho safi kuwa mlezi wa waandishi hao alianza kwa kutembelea maktaba hiyo, kuona shughuli zifanywazo kabla ya kuingia katika kongamano hilo.

Mkurugenzi wa huduma za maktaba taifa Dkt. Mboni ambaye alikuwa mmoja wa wageni maalumu siku hiyo, alimshukuru na kumpongeza mkutubi kiongozi wa maktaba ya Mkoa wa Iringa kwa juhudi zake za kukutanisha waandishi hao.

Aidha alieleza kuwa bodi ya maktaba Tanzania ni taasisi chini ya Wizara ya Elimu yenye lengo la kutoa fursa kwa wote kutumia maktaba za umma. Pia alisisitiza kuwa bodi ya maktaba inahitaji waandishi wa ndani na kuwataka Watanzania waachane na kusoma stori za udaku.

Kongamano hilo pia lilihudhuriwa na mtaalamu wa maswala ya ISBN na ISSN Bi. Irene Moshi kutoka Maktaba kuu ya taifa, Bi. Mwanahamisi Jokolo kutoka TAI na Stanslaus Kigosi, Afisa Hakimiliki kutoka COSOTA. Wote hawa walieleza maswala mbalimbali yanayohusiana na mwandishi na uandishi kwa ujumla.

Wasomi mbalimbali waliohudhuria kongamano hilo waliwasilisha mada anuai kuhusiana na uandishi wa vitabu na majarida.



**Mkuu wa Mkoa wa Iringa (mwenye suruali ya buluu) akiwa katika picha ya pamoja na wakufunzi wa kongamano hilo.**

**Penda kusoma vitabu**

JAMVI la SIMULIZI
www.richardmwambe.com

**Faida za kusoma vitabu:**

- Msisimko wa Akili
- Kupunguza Msongo wa Mawazo
- Kuongeza Ujuzi wa mambo mbalimbali
- Kuongeza Msamiati
- Huboresha Uwezo wa Kukumbuka
- Hukupa Uwezo Mkubwa wa kuchambua na kufikiri
- Huboresha Mtazamo na Umakini

# MREJESHO: Mwanamke Mwandishi

JUZI, Machi 12, nilialikwa na kubahatika kuwa mmoja wa wazungumzaji wachache (Panelist) katika jukwaa la "Recognize Women Authors of Tanzania" hapo Coral Beach, ikiwa ni sehemu ya kumsherehekea "Mwanamke Mwandishi" ndani ya Wiki ya Siku ya Wanawake duniani.

Huku mada kuu ikiwa ni: "The Economic empowerment of Women Author's: How do we grow as women authors in Tanzania!" tulijadiliana mambo mengi yenye shabaha kuu ya kuboresha tasnia ya uandishi.




Mgeni rasmi alikuwa Profesa Penina Muhando, ambaye mbali ya kuwa mwandishi mwanamke, lakini pia alichapisha kitabu chake cha kwanza akiwa binti wa miaka 24 tu. Kwa uzoefu wake mkubwa na weledi wa kutosha, Profesa Penina alitufunda vya kutosha waandishi wa kike kuweza kuendelea kuandika bila kujali wingi wa changamoto unaotukabili.

Mwishoni kabisa, waandaaji wa jukwaa hili, Ellite Bookstore walitutunuku Waandishi Wanawake, vyeti vya utambulisho (Certificate of Recognition) kama sehemu ya kutambua na kuthamini mchango wetu katika jamii. Nawashuru sana.

Ningependa kutoa rai kwa waandishi wa kike kuandika pasi hofu na kutumia muda wao katika kujielimisha na kutafuta maarifa kwa yale wanayoandikia.

***Lilian Mbaga,***

***Machi 15, 2022***

# Je; kusoma ni muhimu katika maisha yetu? - 6



**WAPI NA WAKATI GANI WA KUSOMA KITABU?**

Hili ni swali linalowakuta watu wengi sana, hasa wale wasiosoma vitabu lakini wanapenda. Shida tu kwao ni ile, wakati gani nitasoma? Kutokana na shughuli zetu za kila siku kutunyima muda wa kufanya hivyo unakuta mtu mwingine ananunua vitabu lakini hasomi, anavirundika ndani.

Sikia rafiki, kusoma kitabu ni popote unapoona pana utulivu na ni wakati wowote unaoona unafaa. Kwenye daladala ukipata siti, wakati wa mapumziko uwapo kazini, chooni kwa wale wenye vyoo vya kisasa, popote unapopata muda na nafasi. Siyo lazima uwe na saa sita au saba.

Anayependa kusoma daima utamkuta na kitabu, ama kwenye mkoba wake au tu mkononi. Kwa ulimwengu wa kisasa wa dijitali utamkuta labda na kifaa maalum cha kusomea vitabu cha Amazon (kindle), au simu janja yenye *appilication* hiyo. Kwa mtindo huo anaweza kutembea na vitabu zaidi ya mia moja kwa njia ya kielektroniki.

Kama tulivyosema huko nyuma, kitabu huleta maarifa na kusoma ni kuzaliwa upya, kwa nini uone aibu? Eti nitaaonekana *bishoo* na kitabu mkononi! Hakuna kitu kama hicho. Kila atakayekutazama atapata mguso wa pekee moyoni.

Tunalia ajira hakuna lakini mafunzo mengi ya ujasiriamali yapo vitabuni. Umeshawahi kununua kitabu cha ufugaji kuku? Au ufugaji nguruwe au sungura au hata vile vya kilimo na kusoma? Na ukiisha kusoma ujaribu kufanya vile walivyoelekeza. Hakika utaona mabadiliko makubwa sana katika maisha yako.

Mtaala wa shuleni hautoshi *kukutoa* kimaisha bali siri za maisha zimefichwa kwenye vitabu vya ziada. Soma ukomboke. ***RM***

# RAFIKI BORA NI VITABU—01



Na: Joshua Golyama

*Elimu Kitaa Foundation*

**Habari yako rafiki yangu, Ni matumaini yangu kwamba u mzima wa afya kabisa.**

Karibu katika mfulululizo wa makala hizi kutoka katika kitengo cha KUTOKA VITABUNI.

Ili kuweza kuwa bora katika maisha yako ni vyema sana ukaambatana na kuzungukwa na watu walio na kile ambacho wewe unataka kuwa. Ni asilimia 85 ya mafanikio yako huchangiwa na watu wanaokuzunguka.

Marafiki zako, ndugu zako na jamaa zako ambao unatumia muda mwingi kuwa nao kazini, shuleni, ofisini na maeneo mbalimbali ni muhimu wakachunguzwa na kuona kama wanaweza kukupeleka kule ambako unataka kufika.

Upo msemo wa Kiswahili ambao huzungumzwa kwamba ukitembea na mwizi na wewe utakuwa mwizi, hii humaanisha kwamba ukiambatana na mtu mwenye tabia fulani, *automatically* kuna baadhi ya mambo ambayo utayavuta kutoka kwa rafiki yako.

Eneo hili ni muhimu sana kwa sababu linachangia kwa kiwango kikubwa katika mafanikio yetu na katika safari ya kufika kule ambako tunatamani kufika.

Neno la Mungu linathibitisha hili; tuangalie mifano michache hapa;

**Mithali 13:20** *"Enenda pamoja na wenye hekima, nawe utakuwa na hekima. Bali rafiki wa wapumbavu ataumia"*

**Mithali 22:24-25** *"Usifanye urafiki na mtu mwenye hasira nyingi; wala usiende na mtu wa ghadhabu nyingi;*

*Usije ukajifunza njia zake; na kujipatia nafsi yako mtego.*

**Mithali 27:19** *"Kama uso ufananavyo na uso katika maji; Kadhalika moyo wa mtu na mwenzake"*

**Mithali 27:17** *"Chuma hunoa chuma; Ndivyo mtu aunoavyo uso wa rafiki yake"*

Kutoka kwenye mifano michache ambayo tumeiona hapo juu tunajifunza mambo ambayo hutokea pale tunapokuwa tunaambatana na wale marafiki zetu, familia na wengine na matokeo yake kuwa kama wao.

Mfalme Sulemani anatufundisha hapa kwamba kamwe usifanye urafiki na mtu mwenye hasira kwa sababu unaweza kujifunza pia na wewe.

Unapokuwa unatumia muda wako mwingi na rafiki yako, kuna kuambukizana tabia kunatokea. Hivyo kuna baadhi ya mambo mtaanza kufanana katika mitazamo na hata utendaji wake.

Tunajifunza pia kwamba ili kuwa mtu mwenye hekima ni lazima uambatane na wenye hekima, utumie muda wako mwingi na watu wa aina hiyo.

Najua unayo ndoto ambayo unatamani kuitimiza katika maisha yako, jambo la muhimu sana ambalo unatakiwa kuwa nalo makini ni AINA YA MARAFIKI utakaoambatana nao. Bila shaka utapaswa kuwa makini hasa kuchunguza mitazamo waliyo nayo, na hata ndoto zao, misimamo yao na kuona kama inafanana na wewe na kukusaidia kukuvusha sehemu moja kwenda nyingine katika safari ya mafanikio yako.

Moja ya marafiki ambao unaweza kuwachagua kuambatana nao na ukatumia muda wako mwingi ni VITABU. Najua utashangaa hapa kidogo lakini ambatana na mimi katika kusoma makala hii utajifunza na kujua hasa kwanini kuambatana na VITABU.

Waliotutangulia walijihusisha katika mambo mengi sana, kuna mahali walifanya vizuri sana, kuna mahali walifanya vibaya na hayo yote wameyaandika kwenye VITABU. Naweza kusema kuwa Kitabu ni moja ya hazina kubwa sana ambayo wazee wetu wa zamani walituachia, na hata sisi tunawaachia na tutawaachia yale tunayoendelea kujifunza kila siku. ***Itaendelea...***

# VIRGINIA HALL, MWANAMKE ASIYE NA UMUHIMU—03

**Na Mwandishi wetu**

**William Donovan, chifu wa OSS, alimpatia nishani ya huduma maalum – alimfanya kuwa mwanamke raia wa kwanza kupokea katika Vita ya Pili ya Dunia. Mama yake Hall alikuwa mtu pekee kutoka nje kuhudhuria sherehe hiyo.**

"Sifikiri kwamba amekuwa jasusi mkubwa wa Kimarekani wa Vita ya Pili ya Dunia," Gralley alimzungumzia Hall.

Hall alijiunga na CIA, na kufanikiwa kwenye OSS, alifanya kazi hapo kwa miaka 15, na mara nyingi alikuwa Makao Makuu. Hizi hazikuwa siku zake za furaha. Alikwishazoea kufanya kazi zake katika uwanja wa vita. Sasa muda mwingi aliutumia mezani.

"Kadiri unavyopanda juu kwa cheo, ni pesa na heshima na mipango na sera na yale yote yanayohusu urasimu," anasema Randy Burkett, mwanahistoria wa CIA.



Na Hall alipambana na ubaguzi kama mwanamke..

"Alitendewa vyema? Vizuri, ila kwa kiwango cha sasa, hapana, hakutendewa vizuri," Burkett anaongeza kusema.

Hall alistahafu mwaka 1966 na kamwe hakuzungumza kitu hadharani. Alifariki mwaka 1982 huko Maryland, habari zake zilifungiwa kwenye jumuia ya wanaintelijensia.

Purnell amesema, ilikuwa ni changamoto kuziweka habari zake pamoja.

"Ilikuwa kazi ya kipelelezi," ameeleza. "Makabrasha mengi, karatasi, na maandiko mengine mengi yamepotea, kuharibiwa au kuhifadhiwa vibaya. Amefanya kazi kwa utambulisho na majina tofautitofauti ambavyo watu hawakuweza kumtambua kirahisi."

Sasa vitabu vipo kwenye rafu. Filam zinakuja. Na pale CIA, panajengwa jengo litakaloitwa 'The Virginia Hall Expeditionary Center' .

***MWISHO***



***MWANAMKE ASIYE NA UMUHIMU***

***Imetafsiriwa kutoka katika mtandao na kuletwa kwenu na mwandishi maalum.***

***Katika toleo lijalo atawaletea tena Makala nyingine nzito tamu itakayoukonga moyo wako.***

***Hakikisha unajipatia nakala yako ya Ngurumo ya Mwandishi ili uburudike.***

# TAMASHA LA FASIHI YA KISWAHILI KUFANYIKA NOVEMBA 2022.

**Na Mwandishi wetu**

TAMASHA la pili la Fasihi ya Kiswahili nchini linalotarajiwa kuwaleta pamoja wadau mbalimbali wa fasihi kutoka ndani na nje ya nchi linatarajiwa kufanyika Novemba Mwaka huu.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano ya Umma wa TAFF, Stallone Joyfully, tamasha la mwaka huu linatarajia kupata wageni kutoka nchini Ghana, Nigeria na Kenya na litafanyika kwa siku mbili tofauti na Tamasha la mwaka 2021 ambalo lilifanyika kwa siku moja.

"Tamasha la pili la Fasihi ya Kiswahili litafanyika tarehe 19 na 20 katika Uwanja wa wazi utakaotangazwa baadae ambao utakuwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe mkoani Pwani, ikiwa na kauli mbiu ya

**'KUSOMA, SIACHI NG'O!'** "

Ilisema taarifa hiyo.

Joyfully aliongeza kuwa wadau wote wa fasihi wanaopenda kushiriki wanaweza kuanza kujiandikisha kutokea sasa kwa kutuma barua pepe ya kuomba kushiriki katika anwani ya barua pepe ya TAFF ambayo ni:

fasihifund@gmail.com

Mkuu huyo wa Idara ya Habari na Mawasiliano ya Umma wa TAFF, alisema Tamasha hilo linalofanyika mara moja kila mwaka lina malengo kadhaa mojawapo likiwa ni kuwaleta pamoja wadau wa fasihi na jamii ili kujadili namna bora ya kufanya fasihi kuwa zana muhimu ya maendeleo ya jamii.



Stallone Joyfull kushoto na Hussein Wamaywa kulia wakijadili jambo Wakati wa tamasha la kwanza la Kiswahili lilipofanyika Septemba Mosi, 2021 katika Uwanja wa TRC Chanzige, Halmashauri ya Wilaya ya Kisaarawe mkoani Pwani.

Alisema Tamasha linalenga kurejesha ari ya Jamii kupenda kusoma vitabu ikiwa ni pamoja na kujenga uwezo kwa watunzi wa kazi za kubuni, kubuni kazi za fasihi zenye tija na maslahi kwa jamii zao.

Joyfully alisema, malengo mengine ni kutoa tuzo za umahiri kwa kazi za fasihi ya Kiswahili zilizozofanya vizuri mwaka 2022 kwa wanafunzi wa Shule za Msingi na Sekondari, kufanya uzinduzi wa hadithi za wanafunzi walioshinda mwaka 2021 na kufanya maonyesho na mauzo ya vitabu.

Alisema, Tamasha litatumika pia kuchangia vitabu kwa ajili ya maktaba ya Shule ya Msingi na Sekondari, kuzindua riwaya za aina mbalimbali, kufanya utalii wa kifasihi na kuwakumbuka wanafasihi waliofanya kazi iliyotukuka ambao kwa sasa wametangulia mbele ya haki.

Alitoa wito kwa makampuni ya kibiashara na wadau wengine kujitokeza kudhamini shughuli mbalimbali za Tamasha hilo ili kupata fursa ya kujitangaza na kuuza bidhaa zao kwa kuwa Tamasha la sasa linatarajia kukutanisha wadau zaidi ya 500 wa fasihi kutoka Tanzania na nchi kadhaa za kiafrika

Tamasha la Fasihi ya Kiswahili huandaliwa na Taasisi ya Tanzania Fasihi Fund (TAFF) iliyopo Kisarawe, kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa fasihi ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe mkoani Pwani.

# MPIGA MBIO — 06



Richard Mwambe

**Ilipoishia...**

**"Anhaaaa nimekukumbuka, nilikuwa nakuwaza sasa hivi!"**
**"Jamani, unaniwazia nini eti?" Ikunda akauliza huku akihisi kijinguvu kidogo kimemwingia.**

**Endelea...**

"Nilikuwa nawaza tu huyu mrembo mbona yu kimya!"
"Nipo… maagizo yako niliyafanyia kazi, subiri meseji tu utapata…"
"Asante sana!"
"Haya kaka kwaheri…" ile simu ikakatika.
Ah! Kenneth akajikuta akishangaa na kuitazama simu yake kwenye kioo kana kwamba aliyekuwa akiongea naye angemwona humo. Akakata shauri na kuipiga ile namba. Ikapokelewa.

"Ikunda! Mbona umewahi kukata simu?"
"Mmm kifurushi changu kinaisha…" Ikunda akajibu kutoka upande wa pili.
"Kwanza asante sana, meseji nimeshapata… lakini bibie kuna uwezekano wa kukuona jioni hii? "
"Mmmmmh! We kaka!"
"…au shemeji mkali?" Kenny akauliza kwa kumtega. Ijapokuwa hakuwahi kumuona mara nyingi lakini moyo wake ulimdunda alipomwona pale ndani ya benki. Mara baada ya kuipokea simu yake, akaona ni nafasi kwake kutupa ndoano na hapo alikuwa akisubiri mvuo.
"Hamna! Wala sijaolewa…" upande wa pili ukajibu.
"Mimi nipo hapa Mlimani City, mgahawa wa Samaki Samaki, unaweza kuja?" Kenneth akasubiri jibu huku kiroho kikiruka tiktak.
"Huko mbali lakini…"
"Chukua taksi Mimi nitalipa…" ukimya wa sekunde kadhaa ukajidai kati yao.
"Sawa, basi kama nusu saa tu…"
"Poa!" Kenneth akapiga ngumi mezani. Amefaulu jaribio la kwanza. Alijitahidi kutumia nguvu kumnasa mwanamke huyo kumbe hakujua tu nini kipo moyoni mwa huyo amtaabikiaye. Laiti angejua, ingekuwa kama kuua tembo kwa ubua.

Alipokuja mhudumu kumsikiliza akamwambia asubiri mgeni wake afike. Kenneth hakupenda mazoea na wanawake. Maisha yake alipenda kuyajenga peke yake. Hata alipokuwa na wenzake kikazi hakuwa mtu wa maneno mengi. Mngeweza kukaa nusu saa akaongea maneno matatu kama si matano. Hali hii aliirithi kwa baba yake na kukolezwa katika masomo yake huko seminari. Katika shile hizi za misheni vijana hufundishwa kuwa wanyamavu. Husisitizwa kuwa mwanadamu yakupasa kuwa mnyamavu kwa maana kwenye maneno mengi hapakosi uovu.

…………..

Ilimchukua Ikunda dakika kumi kuwasili pale Mlimani City. Huku moyo wake ukimwenda mbio kama mshale wa saa mbovu, aliteremka kwenye lile taksi na kumlipa dereva shilingi elfu tano. Alisimama, akajishika kifuani upande wa moyo. Kila mara alikuwa akishtukashtuka kama mtu anayedaiwa vikoba. Akamfata mlinzi aliyekuwa akifungulia magari na kumuuliza ni wapi ulipo huo mgahawa. Akaelekezwa.

Akiwa anavuta hatua kuuelekea mlango mkubwa wa kioo, simu yake ikaita. Alipoitazama namba, aliijua. *Habibu!* Alijikuta akisema ndani ya moyo wake.

Habibu ni askari polisi wa FFU ambaye Mara nyingi alikuwa akilinda katika benki hiyo anayofanya kazi Ikunda. Alikuwa shababi, mrefu wa kimo. Habibu alimpenda sana Ikunda, alikwishamtongoza mara kadha wa kadha lakini binti huyo hakutaka kabisa kuwa naye. Jambo hili lilimuuma sana kijana huyu lakini alishindwa afanye nini. Ikunda si tu kwamba hakumpenda huyo kijana bali hakuwapenda polisi, hakutaka kabisa urafiki na polisi na pia hakuwa na tabia ya kuwa na wanaume asiye na lengo naye. Mapenzi yasiyo na tija ni sawa na upatu uvumao. Ikunda hakutaka hili, alihitaji mwanaume wa kujenga naye maisha.

***Itaendelea...***

Riwaya ya
MPIGA MBIO
inatarajiwa kuwa katika mfumo wa kitabu. Weka oda yako sasa kupitia
0766974865

# KIROBA CHEUSI

**Imeandikwa na Omar Kanyaki**

Baada ya kuisoma simulizi ya KIROBA CHEUSI iliyoandikwa na Laura Pettie, nikakumbuka hakuna msichana aliyezaliwa kahaba. Masaibu ya maisha ndiyo yanayopelekea mtu kufanya asiyoyatarajia. Pia mwandishi alituonesha kuwa hakuna kazi rahisi, pale Morena alipomwambia Fatumata "MIE NIECHOKA, MAANA MWINGINE KWA ELFU KUMI YAKE , ANATAKA ANG'OKE NA KIZAZI CHAKO. Pia akatueleza kuwa KAHABA HAKUTAZAMI KAMA MPENZI BALI MTEJA WAKE WA KUDUMU.

Hekaheka ya KIROBA CHEUSI ilisababisha Morena na Fatumata, washike Msahafu kwa Tasbihi na Biblia kwa Rozali. "SHIDA ZINATANABAISHA MWENYE DUNIA HII NI NANI"

Kuna muda nilikaribia kumwaga chozi pale Morena alipotoa maneno makali kwa mtoto wa bosi wake baada ya kuona visa na chuki imezidi. "HATA KAMA UNANICHUKIA ZAIDI YA SHETANI, BADO MIMI NI MWANADAMU, HATA KAMA UNANIONA NI TAKATAKA ….. MIMI NI BINADAMU NINAEFIKWA NA MITIHANI NA NINAUMIA. NINA MOYO KAKA…. Kisha akajishika kifua NINA MOYO SIO JIWE.

KIROBA CHEUSI kimegusa maisha ya uswahilini kwenye nyumba za kupanga, mwandishi akatuonesha maisha magumu mtu ukimdai utamtafuta KUTWA MARA TATU KAMA DOZI YA PANADO na usimpate. Kisha akatupeleka kwenye maisha ya wanaojiweza, mpaka Morena akamwambia Fatumata "KUNA WATU WANAISHI"

Nilicheka pale Fatumata alipoulizwa UNAISHI WAPI na mtu aliyempigia simu kwa namba ngeni na kujibu HAPAHAPA DUNIANI. WE NANI KWANZA.

Ukiisoma simulizi hii hakika utasadiki kweli Laura Pettie ni "FUNDI MSHONA MANENO".






Laura Pettie
Mwandishi wa Kiroba Cheusi

**LAURA PETTIE**

Mwandishi mahiri wa riwaya Tanzania. Amekwishachapisha vitabu viwili; Dira ya Moyo na Kiroba Cheusi.

Zaidi ya vitabu , ni mwandishi anayeandika mambo mbalimbali ya kijamii hususan ushauri na maswala ya kimaendeleo. Mara kadhaa amekuwa mshauri mzuri katika mambo ya kujiwekea akiba 'kibubu' na MAONGEZI YA JIONI.



# Tangazo

**MADUKA NA WAKALA WA VITABU NCHINI**

1-KONA YA RIWAYA
Kinondoni Morrocco
Nyuma ya jengo la Airtel
mob: 0655428085

2-POSTA MPYA
Kwa George-
karibu na Askari Monument
mob:0755454152

3-MOROGORO
Bima Samaki Samaki
Mob:0748623743

4-ARUSHA
Nje ya duka la Kimahama
Mob: 0757690302

5- MBEYA
Duka la vitabu
FANANI na HADHIRA
Mob: 0746840840

6-IRINGA
LUTENGANO stationary
Miyomboni

©ngurumo ya mwandishi 2022



JAMVI la SIMULIZI
www.richardmwambe.com

**NGURUMO YA MWANDISHI**

**S.L.P 1039**
**IRINGA—TANZANIA**

**Instagram: jamvi la simulizi**

**Email: jamvilasimulizi"gmail.com**

**Whatsapp: 0734550514**

**Mob: 0766974865**
**0672160016**


## ZAWADI YA PASAKA: JAMVI LA SIMULIZI APP (17/04/2022)




Furahia PASAKA yako na APP yako pendwa itakayoifanya sikuu yako kuwa murua na nyepessi.

APP ya Jamvi la Simulizi iliyosheheni riwayaa pendwa za kijasusi, Makala nzito nzito za kijasusi nk, bila kusahau majarida ya Ngurumo ya Mwandishi matoleo yote na picha za matukio mbalimbali ya Wadau wa Jamvi na maisha yao ya kila siku.

APP hii itakuwa hewani kupitia Play Store kuanzia taarehe 17 ya mwezi wa April mwaka huu.

Hivyo basi, wewe mpenzi wa fasihi ya Kiswahili, hususan riwaya tamu zisizochosha za Kamanda Amata, sasa tumekusogezea kiganjaani mwako.

Pakua, ujisajili, uwe mmoja wa familia kongwe ya Jamvi la Simulizi.

Tunaakusubiri pale.




Imetolewa na uongozi wa Jamvi la Simulizi

© **Rehema Stanley**—Meneja na Msemaji wa Jamvi la Simulizi.